

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Simu: +255-26-2323189

Baruapepe: ps@moha.go.tz

Tovuti: www.moha.go.tz



Mji wa Serikali- Mtumba,

Mtaa wa Habari/Afya,

S.L.P 2916,

40483 DODOMA.

Unapojibu tafadhalii taja:

13 Juni, 2024

TANGAZO

NAFASI ZA KUHAMIA KATIKA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepewa kibali na mwenye Mamlaka Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora cha kujaza nafasi 26 zilizo wazi kwa utaratibu wa kuhamishiwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Kwa kibali hicho Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi anawatangazia watumishi wote wa Umma Tanzania, wenyewe nia na wanaokidhi vigezo vya Kimuundo kuwasilisha maombi kwa ajili ya nafasi za zifuatazo hapo chini:-

- | | |
|--|-----------|
| 1. Msaidizi wa Kumbukumbu Mkuu Daraja II | Nafasi 1, |
| 2. Msaidizi wa Kumbukumbu Mwandamizi | Nafasi 2, |
| 3. Afisa Ugavi Mkuu Daraja la II | Nafasi 1, |
| 4. Afisa Ugavi Mwandamizi | Nafasi 1, |
| 5. Afisa Ugavi Daraja la II | Nafasi 2, |
| 6. Mchumi Daraja la I | Nafasi 1, |
| 7. Mchumi Mwandamizi | Nafasi 2, |
| 8. Mchumi Mkuu Daraja la II | Nafasi 1, |
| 9. Mtakwimu Mkuu Daraja la II | Nafasi 1, |
| 10. Mtakwimu Daraja la I | Nafasi 1, |
| 11. Afisa Ustawi wa Jamii Daraja la II | Nafasi 5, |
| 12. Afisa Hesabu Mwandamizi | Nafasi 1, |
| 13. Afisa Sheria Mkuu Daraja la II | Nafasi 3, |
| 14. Afisa Sheria Mwandamizi | Nafasi 2, |
| 15. Mkaguzi wa Ndani Mwandamizi | Nafasi 1, |
| 16. Mkaguzi wa Ndani Daraja la I | Nafasi 1, |

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI:

- i. Waombaji wote wapitishe barua za maombi kwa Waajiri wao
- ii. Maombi hayo yaambatane na uthibitisho wa Mwajiri kuhusu uhakiki wa vyeti vya kidato cha nne kutoka NECTA
- iii. Waambatishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani zao, namba za simu pamoja na majina ya wadhamini watatu wa kuaminika
- iv. Maombi yaambatane na vyeti vya elimu na taaluma
- v. Mwombaji asiwe na shauri la kinidhamu
- vi. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 30 Juni, 2024
- vii. Mwombaji atajigharamia gharama za uhamisho
- viii. Maombi yawasilishwe kupitia Mfumo wa kielektroniki wa Uhamisho *e-transfer* kwa anuani ya:-

Katibu Mkuu,
Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi,
S. L. P 2916,
40483 DODOMA

Imetolewa na: Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi